

Tamko la HakiElimu Kuhusu Matukio ya Ukatili kwa Watoto Mkoani Njombe

Tumepokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa za matukio ya mauaji ya watoto,hususani wenye umri kati ya miaka miwili hadi sita, yaliyotokea hivi karibuni huko mkoani Njombe. Matukio haya yameambatana na kuchinjwa na kukatwa baadhi ya viungo vya miili ya watoto hao.

HakiElimu tunatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na wakazi wote wa Mkoa wa Njombe kwa mauaji haya ya kutisha. Pia, tunawasihi kuwa wavumilivu katika kipindi hiki kigumu na kuwaomba kutoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama katika uchunguzi wao utakaosaidia kuwabaini wahusika wote ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Aidha, HakiElimu inaungana na watetezi wengine wa haki za mtoto na wataanzania wema kwa ujumla kulaani na kukemea vikali vitendo hivi vya ukatili dhidi ya watoto kwani vimewasababishia watoto hao kupoteza haki yao ya kuishi na kudhalilisha utu wao kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Sheria ya Mtoto na Mkataba wa Kimataifa ya Haki za Mtoto bila hatia yoyote.

Mauaji ya watoto mkoani Njombe yameibua hisia kali kwani yametokea mfululizo yakiambatana na kunyofolewa kwa baadhi ya viungo vyao vya miili yao. Matukio mengine ya ukatili dhidi ya watoto yameripotiwa kutokea katika maeneo mengine nchini yakihusisha utekaji, ubakaji, kupotea na mauaji. Ni dhahiri kuwa usalama wa watoto wetu sasa uko hatarini. Aidha,hata hii haiko tu majumbani, bali hata kwenye maeneo mengine kama vile hospitalini, shuleni, mitaani, mashambani na hata katika nyumba za ibada!

Tunaishukuru Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa kuchukua hatua za haraka kutaka kubaini chanzo na wahusika wa matukio haya ili kuwachukulia hatua za kisheria mapema iwezekanavyo.

Ingawa tayari vyombo vya ulinzi vimeanzisha msako wa wote wanaohusishwa na vifo hivi, bado kuna haja ya kuimarisha ulinzi wa watoto wetu kwani ulinzi na usalama wa watoto ni jukumu letu sote.

Kwa kumalizia, HakiElimu inapendekeza mambo yafuatayo:

1. Serikali, jamii na wadau wote tuzidi kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto wetu nyumbani, shuleni, hospitalini, nyumba za ibada na maeneo yote ambayo watoto hukusanyika ama hukaa huko kwa muda mrefu.
2. Serikali iweke mipango endelevu ya kuimarisha mifumo rasmi ya ulinzi na usalama wa watoto shuleni, nyumbani na maeneo mengine.
3. Serikali na wadau wengine wote hususani viongozi wa dini wazidi kutoa elimu kwa umma ili watu waondokane na imani potofu kuwa mafanikio yanaweza kupatikana kwa kupiga ramli au kutumia viungo vya binadamu!
4. Serikali iongeze kasi ya uchunguzi wa matukio haya na kuwachukulia hatua kali wote watakaobainika kuhusika na vitendo hivyo vya ukatili dhidi ya watoto ili kukomesha uovu huu.

Dkt John Kalage
Mkurugenzi Mtendaji, HakiElimu